

## **“Biblia yasemaje.....”**

### **Yesu aliachukuliaje maandiko?**

#### **Sehemu ya Tano**

“Tena kwa habari ya kiyama ya watu, hamjalisoma neno lililonenwa na Mungu, akisema, mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? Mungu si Mungu wa wafu, bali wa walio hai” (Mathayo 22:31-32).

“Tena akasema, Mimi ni Mungu wa Baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo,” (Kutoka 3:6).

Katika Mathayo 22:23-33, twaona mfano mwingine jinsi Yesu alivyotumia maandiko. Alitumia sarufi ya aya ili kuthibitisha anachomaanisha. Yesu alikuwa anakabiliana na fundisho potofu lililokuwa limeenea. Masadukayo waliokuwa wanaunga mkono fundisho hili , walimtega Yesu mbele ya umati wa watu kuhusiana na ndoa, kifo, na kiyama.

Yesu alinukuu Kutoka 3:6 ambapo Mungu alimwita Musa ili awaongoze watu wake watoke utumwani. Mungu akajitambulisha kama Mungu wa Amram, Ibrahimu, Isaka, na Yakobo huku akitumia kitenzi cha wakati uliopo. Maana yake ni kwamba Mungu alikuwa anasema hawa watu wanne walikuwa hai, hata ingawa Ibrahimu alikuwa amekufa mamia kadhaa ya miaka nyuma. Naye Yesu katika Mathayo 22:32 alikubaliana kwa kusema walikuwa bado hai. Ndipo Masadukayo wakatambua kuwa njama yao imefeli. Lakini makutano wakabaki waduwazwa na Mwalimu mahiri (Mathayo 22:33).

Kama Yesu, nasi lazima tusome maandiko kwa makini na tuelewe kuwa sarufi ni muhimu ili kikitumia vyema kitabu. Mathalani, twaweza kusoma kuhusu “ubatizo mmoja” katika Waefeso 4:5 na tukaelewa kuwa ubatizo mmoja ndiyo unaokubalika na Mungu. Twaweza kusoma katika Mathayo 16:18, ambapo Yesu alisema “na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu” na kwa kutumia sarufi twaweza kuelewa kuwa kuna Kanisa moja. Kanisa hilo moja ni la Kristo, na kuwa Kanisa la Kristo.

Yesu aliachukukilia maandiko kwa uaminifu na maarifa. Fanya hili liwe kusudi lako. Soma, jifunze na tumia maandiko kwa halali kwa kufuata mfano wa Yesu. Tena, la muhimu zaidi ya yote, unapowasikiliza wahubiri na walimu, wianisha wanavyoyatumia maandiko na namna Yesu alivyoyatumia maandiko.